

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA**

**20 MEI, 2019**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA – TAREHE 20 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**252. MHESHIMIWA TAUHIDA CASSIAN GALOSS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro wa muda mrefu kati ya Kituo cha

Polisi Bububu na Soko dogo la Wananchi lililopo karibu na Kituo hicho;

(b) Je, kiutaratibu umbali kati ya Kituo cha Polisi na Makazi ya Wananchi ni hatua ngapi.

**253. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Pamoja na jitihada za Vijana wengi kujiajiri wenyewe kwa kuendesha bodaboda wamekuwa wakisumbuliwa na Polisi kwa pikipiki zao kukamatwa mara kwa mara:-

Je, kwa nini pikipiki zao zinapokamatwa na wanapoenda kuzichukua hukuta baadhi ya vifaa kama betri hazipo.

**254. MHESHIMIWA RITHA ENESHER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Tangu Wilaya ya Kilolo ipate hadhi ya kuwa Wilaya mwaka 2002 Serikali haijaweza kujenga Ofisi za Polisi na Nyumba za kuishi yalipo Makao Makuu ya Wilaya:-

Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi na Nyumba hizo za Polisi Wilaya ya Kilolo.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **255. MHESHIMIWA DKT. DALALY PETER KAFUMU (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-  
Mwaka 2018 ulikuwa msimu wa mvua nyingi sana zilizosababisha kubomoka kwa Mabwawa ya maji kwenye Kata za Kinungu, Nguvumoja, Mwamashimba, Nanga, Bukoko na Mbutu na kuwaacha Wananchi wa Vijiji zaidi ya 24 bila maji; Maeneo haya ni mbuga na hayana maji chini ya ardhi hivyo Wananchi hutegemea Mabwawa hayo tu. Aidha, Halmashauri ya Igunga haina uwezo wa kifedha kuyakarabati Mabwawa hayo mara moja:-

Je, ni kwa nini Serikali isilete mradi mkubwa wa kukarabati miundombinu ya maji katika Kata hizo ili kuwaondolea Wananchi hao tabu ya maji.

### **256. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA KITANDULA (MKINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini mradi wa maji kutoka chanzo cha Mto Zigi kwenda Mkinga na Horohoro utaanza.

**257. MHESHIMIWA RICHARD MGANGA NDASSA (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Sumve, Malya hadi Malampaka ambao usanifu wake umeshakamilika ni ahadi ya Mhe. Rais:-

Je, ni lini mradi huo utatekelezwa.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**258. MHESHIMIWA ENG. RAMO MATALA MAKANI (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

- (a) Je, Ikama ya Wataalamu wa Ardhi Katika Halmashauri za Wilaya ni ipi na ni lini Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru itafikia kiwango hicho;
- (b) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kurudisha eneo la Hekari takriban 2,000 za Shamba Pori la Nambarapi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ili nayo

irejeshe ardhi hiyo kwa Wananchi wa Vijiji husika kikiwemo Kijiji cha Nambarapi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**259. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE MWAMBALASWA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Chunya ni moja kati ya Wilaya 10 nchini zilizopangiwa kujengewa Chuo cha VETA mwaka 2013:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo hicho.

**260. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Walimu wenye weledi wa kuwafundisha Watu Wenye Ulemavu ni wachache sana nchini:-

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha Walimu hao ni wa kutosha.

**WIZARA YA NISHATI:**

**261. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA  
THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Megawati moja ya umeme inazalishwa kwa bei gani na inauzwa kwa bei gani (*unit cost*).

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA KILIMO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**(Majadiliano yanaendelea)**

**DODOMA  
20 MEI, 2019**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**